KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 16, Issue 3

22nd Dhul Hijjah 1432

18th Nov, 2011

YALIYOMO

SHERH AQEEDAT... 1 - 3

KUKIDHI HAJA 3 - 4

SHERH 'AQEEDAT AT-TAHAAWIYYAH (PRT II)

Dr: Muhammad bin Abdur-Rahman al-Khumayyis

MLANGO WA TATU:

[13] Hakuwahi kukosekana kuwepo pamoja na sifa zake tangu kabla ya kuumba. Kuwaleta kwake viumbe haikumzidishia kitu chochote ambacho hakikuwepo katika sifa zake. Na kama Alivyokuwa, pamoja na sifa Yake ya Utangu (.أزليًا)Vilevile ataendelea kuwepo daima na milele.

Hakika kila sifa miongoni mwa sifa za Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) ni zenye kuuthibitisha Utangu wake (kuwepo kwake), tangu hata kabla ya kuwaumba viumbe vyake. Na hizo zote ni sifa za ukamilifu ambazo zikikosekana huwa pana kasoro. Kwahivyo hapana budi kwa Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) kusifiwa kwa sifa za Ukamilifu badala ya sifa zilizo na upungufu. Sifa hiyo haiukumstahiki Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) baada ya kuwaumba watu, **bali sifa Zake zote zimethubutu juu yake kabla ya kuwaumba.** Kama ambavyo Yeye (*Subhaanahu wata'aalah*) ni wa Tangu katika sifa zake, hapakuwa na chochote kilichomtangulia, vilevile kuendelea kuwepo daima na milele ni kwake. Hizi ni sifa zisizokuwa na mwisho, bali ni zenye kubakia pamoja na sifa anazosifiwa nazo (*Subhaanahu wata'aalah*).

[14] Haikuwa tu baada ya kitendo cha kuumba viumbe ndio akasifiwa kwa jina la Muumba (,الخالقwala sio baada ya kitendo cha kuanzilisha tu ndio akasifiwa kama "Muanzilishi" (.الباري

Nae Aliyetukuka, alikuwa ni Muumba hata kabla ya kuwaumba viumbe, na alikuwa akiitwa kwa jina hili kabla hajawaumba. Wala hapakua na kikomo cha kuitwa kwa jina hilo baada ya kutekeleza kitendo cha kuwaleta viumbe.

Na pia haitofaidisha kitu iwapo jina la "Muanzilishi" lilipatikana baada ya kuwaleta viumbe, lakini (ukweli ni kwamba) alikuwa ni Muanzilishi hata kabla ya kuwaumba na kuwaleta hapa ulimwenguni. Kwahivyo, jina Lake na sifa Yake hiyo zilikuwepo tangu zamani pamoja na enzi ya dhati yake (*Subhaanahu wata'aalah*). Imethubutu yakwamba Mtume Muhammad (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) amehadithia yakwamba Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*):

Alipitisha makadirio ya viumbe vyake kabla hajaumba mbingu na ardhi kwa muda wa miaka elfu khamsini.

[15] Yeye daima alikuwa ni Mola hata kama hakuwa ni Mola wa kitu chochote, na daima alikuwa ni Muumba hata kama hapakuwa na kiumbe chochote:

Hakika Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) ndiye Mola katika kila maana ya ukamilifu ya Uola hata kabla ya kumuumba mmojawapo wa viumbe vyake. Na vilevile Yeye alikuwa ni Muumba hata kabla ya kuwaumba. Kwahivyo, haya ndiyo majina pamoja na kila ushahidi, miongoni mwa maana zilizothubutu juu yake za kabla na baada.

[16] Na kama ambavyo hakika Yeye ni 'Mwenye kuwahuisha waliokufa' baada ya kuwapa uhai mara ya kwanza, na anastahiki jina hili kabla ya kuwapa uhai, na vilevile anastahiki jina la "Muumba" kabla ya kuwaleta Ulimwenguni:

Kwa hakika Yeye (*Subhaanahu wata'aalah*), kama ambavyo ni Mwenye kuwahuisha (kuwapa uhai) waliokufa baada yakwamba aliwapa uhai hapo mwanzo, vilevile Atawapa uhai waliokufa kabla ya kuwahuisha tena. Na kama ambavyo Yeye (*Subhaanahu wata'aalah*) ni "Muumba" baada ya kuwaumba viumbe vyake, pia alikuwa ni "Muumba" hata kabla ya kuwaumba wao kadhaalika kwa sababu Yeye (*Subhaanahu wata'aalah*) ana Uwezo juu ya kila kitu. Anapotaka jambo lake, hufanya tu bila ya pingamizi yoyote na asipotaka jambo lisiwe, basi haliwi. Na hii ndiyo rada ya maamrisho yenye makadirio ya Mwenyezi Mungu yajulikanayo kama:

(*al-iraadat al-kawniyyatu al-Qadariyyah* (الإرادة الكونية القدرية

Ambayo hakuna chochote kiwezacho kuiepuka, wala kuikwepa kabisa. Wamesema watu wa pote la ***al-Mu'tazilah:*** Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) ni Muweza wa kila jambo ambalo ana uwezo nalo, amma kuhusu vitendo vya waja wake, basi Yeye hana uwezo navyo. Huku ni kuzibambua sifa za Mkamilifu. Kwa hakika Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) ni Muweza wa kila kitu kama Alivyotupasha khabari kuhusu Yeye mwenyewe (*Subhaanahu wata'aalah*):

Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu. [Soorat al-Baqarah 2:284]

[17] Hiyo ni kwa sababu Yeye ana Uwezo juu ya kila kitu, na kila kitu ni chenye kumtegemea Yeye, na kila kitu ni chepesi kwake Yeye, na hakuna chochote anachohitaji. Hakuna chochote mfano wake; naye ni Mwenye kusikiya, Mwenye kuona: Na kadhaalika kila jambo lililoko katika ulimwengu huu basi ni kwa ajili ya irada ya Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) na matakwa Yake. Na kuwa na Imani juu ya masala haya ni miongoni mwa mambo muhimu yanayotulazimu kuamini kuhusu Uola wa Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*). Kila kitu katika kuwepo kwake ni chenye kumtegemea Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) na kuhitaji kutoka kwake ili yabakie kuendelea kuwepo. Na yote hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu, kama alivyosema (*Subhaanahu wata'aalah*):

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

Kwa yakini hilo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu. [Soorah al-Hadyd 57:22]

Na Yeye (*Subhaanahu wata'aalah*) hahitaji kitu chochote kutoka kwao, bali hapana budi yakwamba kila kitu kinamuhitaji Yeye. Mahitaji yao kwa Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) yamethubutu (yako imara), hayabadiliki wala hayawi kulingana na nyakati tafauti, au kulingana na mahali tafauti:

Hakuna chochote mfano Wake; naye ni Mwenye kusikiya, Mwenye kuona. [Soorah ash-Shoorah 42:11]

KWA MUKHTASAR:

Sifa za Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)* za dhati Yake na sifa za vitendo Vyake ni jinsi za zamani sana, hata inapotokea mojawapo. Nayo itaendelea kubaki na Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)*, ambae ndie anaestahiki kulingana na majina Yake na sifa Zake kabla na baada ya kuwaumba.

Masuali:

Jee, maana ya "Uola" wa Mwenyezi Mungu ulihitaji kupatikana viumbe ili awe ndie Mola wao?

Jee, Qadar ya Mwenyezi Mungu inajuzu katika kila kitu?

Ni nini maana ya maneno Yake Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)*:

-Hakuna chochote mfano Wake; naye ni Mwenye kusikiya, Mwenye kuona.?

MLANGO WA NNE:

[18] Amewaumba viumbe kwa 'Ilmu Yake:

Kwa hakika Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)* aliwaumba viumbe vyake na Anawajua vilivyo kama alivyosema:

Oh! Asijue aliyeumba! Naye ndiye avijuaye visivyojulikana na vinavyojulikana. [Soorah al-Mulk 67:14]

Na ilimu Yake *(Subhaanahu wata'aalah)* imekusanya kila kitu, kama alivyosema:

(Mwenyezi Mungu) Anajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala wao hawawezi kumjua (Mungu) vilivyo. [Soorat Taa-ha 20:110]

Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)* anayajua yaliyokuwa na yatakayokuwa, na yale ambayo hayawi lau kama yangelikuwa:

Hakifichikani kwake (kitu chochote hata) kilicho na uzito wa mdudu chungu, katika mbingu wala katika ardhi, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa zaidi; ila (vyote hivyo) vimo katika Kitabu (chake) kielezacho (kila jambo). [Soorat as-Saba' 34:3]

Hakuna chochote chenye kufichika kwake, na 'ilmu Yake *(Subhaanahu wata'aalah)* ni yenye kuhusu kila kitu katika ukamilifu wake wote na kwa sehemu yake.

Na Akawaja'aliya wao Qadar:

Na kila kitu kimeumbwa na Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)* kwa Qadar kama Alivyosema ('Azza wa Jall):

Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kiasi (chake makhsusi). [Soorah al -Qamar [54:49

Na kama alivyosema tena:

Na Ameumba kila kitu na akakikadiria kipimo (chake): [Soorah al-Furqaan 25:2]

Kwahivyo, kheri na shari ni makadirio aina mbili, na kila kitu kimeumbwa kwa Qadar, wamekosolewa kwa ajili hiyo wale wanaodai yakwamba mambo ya shari hayakuumbwa na Mwenyezi Mungu.

Na Akawaekea wao wakati maalum (wa kuishi):

Nae (*Subhaanahu wata'aalah*), kwa yakini Amewaandikia viumbe vyake wakati wao maalum (wa kuishi) na wala hawaongezei muda ukufika:

Utakapowafikia muda wao huo, hawatakawia (hata) saa moja wala hawatatangulia (kabla haujafika). [Soorat al-A'raaf 7:34]

Wala haimkiniki yakwamba kitu chochote kitangulie au kichelewe katika ajali yake ambayo iliyopangiwa kutokea na Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*)

Na hakuna chochote kinachowahusu wao kilichofichika kwake kabla ya kuwaumba wao, na anayajua yote ambayo watakayoyatenda kabla hajawaumba.

Hakika ya jambo hili ni kwamba Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) alikuwa hashindwi kujua kila kitu kabla hajawaumba viumbe vyake. Aliwajua watu wenye ne'ma na wenye maafa, na watu wema na watu waovu, wote hao kabla hajawaumba, na anaendelea kuwajua miongoni mwao katika siku kadhaa wako katika hali kadhaa. Kutakasika ni kwake (*Subhaanahu wata'aalah*) na hapana chenye kufichika kwake katika siri za viumbe vyake.

KWA MUKHTASAR:

Kwa hakika Mwenyezi Mungu *(Subhaanahu wata'aalah)* amewaumba viumbe vyake kwa Ilimu yake, na akakadiria makadirio katika kila kitu. Wala hapana chochote chenye kufichika kwake kutoka kwa viumbe vyake, wala amali zao na hayo yote ni kabla ya kuwaumba.

Masuali:

1.Ni nini maana ya maneno yake: Akawakadiria makadirio?

Jee, Mwenyezi Mungu alikuwa akijua amali za viumbe vyake kabla hajawaumbia (hizo amali)?

MLANGO WA TANO:

Na Akawaamrisha wamtwi'i na Akawakataza kumu'asi Yeye.

Kwa hakika Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*) amewaamrisha viumbe vyake wamtwi'i Yeye, na akawaahidi kwa ajili ya twa'a yao thawabu nyingi sana, na akawakataza kufanya maasia na kuwaonya dhidi ya kufanya (hayo maasia) kwa adhabu kali. Kama alivyosema Mola (*Subhaanahu wata'aalah*):

Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, (Mwenyezi Mungu) atamwingiza katika Bustani zipitazo mito mbele yake; wakae humo milele. Na huko ndiko kufaulu kukubwa. Na anayemwasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kuiruka mipaka yake, (Mwenyezi Mungu) atamwingiza Motoni, humo atakaa milele, na atapata adhabu zifedheheshazo. [Soorah An-Nisaa' 4:13-14]

Na kule kutaja kwake (*Rahimahullaah*) kuhusu maamrisho na makatazo baada ya maneno yake juu ya Kuumba ni ishara yakwamba Muumba ndiye anayestahiki kuamrisha na kukataza kama alivyosema Mwenyezi Mungu (*Subhaanahu wata'aalah*):

Fahamuni! Kuumba (ni kwake tu Mwenyezi Mungu) na amri zote ni zake (Mwenyezi Mungu). [Soorah Al-A'raaf 7:54]

Na kila kitu kinakuwa kulingana na makadirio na Matakwa (ya Mwenyezi Mungu), na Matakwa Yake yanakuwa bila ya pingamizi, Matakwa ya wana-adamu hayawi isipokuwa alowapendelea (Mwenyezi Mungu) liwe. Analotaka liwafike halina budi (kuwafika), na asilotaka liwafike, haliwi.

Na kila kitu kinakuwa kulingana na makadirio na Matakwa ya Mwenyezi Mungu, kwa kupitisha na kukadiria, wala hapana kitu chochote chenye kutokea isipokuwa kwa Matakwa Yake

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

(Mwenyezi Mungu *Subhaanahu wata'aalah*), wala haimkiniki kutokea jambo lolote katika mas-ala haya bila ya Matakwa ya Mwenyezi Mungu *Subhaanahu wata'aalah*. Na Matakwa ya Mwenyezi Mungu *Subhaanahu wata'aalah* yanakuwa bila ya pingamizi

ADABU ZA KUKIDHI HAJA

Na: Sheikh Abdullaah bin Saalih al -Ubaylaan

Kwanza kabisa nitaanza kuyazungumzia yale yanayohusiana na *Wudhoo'* (kutawadha). Lakini kabla ya hayo nitazungumzia kuhusu adabu za kukidhi haja, kama vile haja ndogo (mikojo) na haja kubwa (kinyezi).
Ni jambo la Sunnah kwa Muislamu, pindi anapotaka kukidhi haja yake, ajitenge na watu. Haya yame egemezwa juu ya hadeeth iliyopokewa na Al-Mugheerah bin Shu'bah *(radhiallaahu 'anhu)* aliyesema: **"Amesema Rasoolullaah (sallallaahu 'alayhi wasallam): 'Hebu nishikie hichi chombo (kopo).' Kisha akaondoka kwenda kando mpaka akanipotea machoni mwangu na akakidhi haja yake."** [Imepokewa na Al-Bukhaaree na Muslim].
Na hadeeth hii ni ushahidi yakwamba mtu anapokidhi haja anawajibika kujificha ili asionekane na watu.
Katika Sunan Abu Dawood, kwa upokezi ulio na daraja ya Hassan, Al-Mugheerah bin Shu'bah vilevile akatuhadithia: **"Pindi Rasoolullaah (sallallaahu 'alayhi wasallam) anapotaka kukidhi haja ndogo, huwenda faragha (kuwa kando au mbali na watu)."**
Na katika Sunan Abu Dawood, upokezi wa riwaya kwa njia ya *hasan li-ghayrihi* (inayokubalika kutokana na usaidizi), Jaabir bin 'Abdillaah *(Radhiallaahu 'anhumaa)* akatuhadithia: **"Alipokuwa Rasoolullaah (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) akitaka kukidhi haja, huenda sehemu iliyo kando mpaka akawa haonekani na mtu yoyote."**
Vilevile imependekezwa kwa Muislamu, kabla hajaingia chooni, iwapo ni ndani ya jengo au nyumba au sehemu ya nje, aseme kabla hajaingia chooni au anapokaa nje: ***"Allaahumma Innee 'Audhu bika min-al-khubuthi wal-khabaa'ith."*** [Ewe Allaah, hakika (yangu mimi), najilinda Kwako kutokamana na mashetani wanaume na mashetani wanawake]
Hayo yametokamana na hadeeth iliyopokewa na Al-Bukhaaree na Muslim kutoka kwa Anas (*radyAllaahu 'anhu*) yakwamba alisema: **"Kila Mtume anapoingia chooni, husema: "*Allaahumma Innee 'Audhu bika min-al-khubuthi wal-khabaa'ith*."** [Ewe Allaah, hakika (yangu mimi), najilinda Kwako kutokamana na mashetani wanaume na mashetani wanawake]
Maana ya **"*'Audhu bika*"** ni: Najilinda Kwako. **"*Al-Khubuth*"** maana yake ni mashetani wanaume na **"*Al-Khabaa'ith*"** maana yake ni mashetani wanawake. Kwahivyo kila mtu hujilinda kwa Allaah kutokamana na uovu wao. Na sababu ni kwamba sehemu hizo za chooni ni makaazi ya mashetani, kama isemavyo riwaya ya Zayd bin Arqam (*radhiAllaahu 'anhu*) katika Sunan Abu Dawood, aliposema yakwamba Rasoolullaah (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) amesema: **"Kwa hakika, hizi sehemu za vyoo zina wenyeji. Kwahivyo anapoingia mmoja wenu chooni, basi na aseme: '*Allaahumma Innee 'Audhu bika min-al-khubuthi wal-khabaa'ith* .'"** Upokezi wa riwaya yake ni saheeh.
Mtu na aseme **"*Bismillaah*"** kabla hajasema **" *Allaahumma Innee 'Audhu bika min-al-khubuthi wal-khabaa'ith*"** kutokana na riwaya iliyopokelewa na 'Alee (*radhiAllaahu 'anhu*) aliyesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*): **'Sitara iliyoko baina ya Jinni na sehemu za tupu za mja, ni kuyatamka maneno haya: *Bismillaah* (Kwa jina la Allaah).'** " Imepokewa na At-Tirmidhee na Ibn Maajah na upokezi wa riwaya hiyo ni wenye kukubalika (*hasan*) kutokana na usaidizi wa kushuhudiwa.
Mtu na asiinue (asipandishe juu) nguo zake mpaka achotame kwenye ardhi, kutokana na yaliopokewa na Al-Bayhaqee kwa upokezi mzuri (*jayyid*) wa riwaya kutoka kwa Ibn 'Umar (*radhiAllaahu 'anhumaa*) yakwamba: **"Rasoolullaah (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) hakuwa akinyanyua nguo zake mpaka achotame chini kwenye ardhi."**
Vilevile, alikuwa akijiekea kizuizi baina yake na macho ya watu, kulingana na yale aliyoyapokea Abu Dawood kutoka kwa 'Aa'ishah (*radhiAllaahu 'anhaa*) kwa upokezi wa riwaya iliyo hasan kulingana na Al-Haafidh Ibn Hajr, yakwamba alisema ('Aa'ishah): "Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*): **'Yeyote mwenye kutaka kukidhi haja, basi na ajisitiri.'"** Pia ime egemezwa juu ya yale aliyoyapokea Muslim kutoka kwa 'Abdullaah bin Ja'far, yakwamba amesema: **"Alikuwa Mtume (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) anapokidhi haja yake akipenda kwenda kwenye sehemu pana iliyo na vizuizi vya kujisitiri au boma liloezekwa makuti ya mtende."**
Na imeharamishwa kwa Muislamu kukidhi haja yake njiani, kwenye mapito ya watu au katika sehemu ya kivuli, ambapo watu hufanya kuwa maskani yao ya mapumziko. Hii imetokana na riwaya iliyopokewa na Abu Hurairah (*radhiAllaahu 'anhu*) kutoka kwa Mtume (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) kuwa amesema: **"Jihadharini na mambo mawili yenye kumsababisha mtu kulaani (laana za watu zisiwashukie). Yule mwenye kukidhi haja katika barabara au kwenye sehemu zao za vivuli."** Imepokewa na Muslim.
Kwa ujumla hii inahusu kitu chochote kinachotumiwa na watu, iwapo ni barabarani, baadhi za sehemu zenye vivuli, au kwenye sehemu zenye miti yenye matunda au kwenye sehemu zao za maji (yaani: kwa usafishaji). Haijuzu kwake yeye kukidhi haja yake katika sehemu hizi, kwa sababu atayasababisha kuwa najisi kwa waislamu wengine.
Vilevile imeharamishwa kwa Muislamu kukielekea au kukipa kibla mgongo pindi anapoqidhi haja yake, haswa zaidi anapokwenda haja kubwa (kupata choo). Hii imetokana na riwaya aliyoipokea Abu Ayoob Al-Ansaaree (*radhiAllaahu 'anhu*) kutoka kwa Mtume (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) yakwamba amesema: **"Unapokwenda kukidhi haja (kubwa), basi usielekee Qibla wala usikipe (Qibla) mgongo. Badala yake geuka (na uelekee) Mashariki au Magharibi."** Na hadeeth hii imeafikiwa (na Bukhaaree na Muslim). Na zaidi ya hayo ni kwamba hadeeth hii imewahusu watu wa Madeenah kwa sababu kwao wao, Qibla ni kuelekea kusini.
Pia hii imetokamana na riwaya aliyoipokea Muslim kutoka kwa Abu Hurairah (*radhiAllaahu 'anhu*) yakwamba Rasoolullaah (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) amesema: **"Anapochotama mmoja wenu kukidhi haja yake, basi na asielekee (upande wa) Qibla wala asikipe mgongo (Qibla)."**
Amma kuhusiana na suala la istinjaa, ambalo ni kujisafisha (au kunawa) kwenye tupu ya mbele au nyuma baada ya kumaliza kukidhi haja, basi Muislamu

(Endelea kutoka Uk. 3)

ana khiyari ya kuchagua baina ya kutumia maji au mawe katika kutekeleza istinjaa. Kwahivyo iwapo atafaulu kujitahirisha kwa maji, basi istinjaa yake itajuzu, kutokamana na riwaya iliyopokelewa na Al-Bukhaaree na Muslim kutoka kwa Anas (*radhiAllaahu 'anhu*) yakuwa amesema: **"Rasoolullaah (*sallAllaahu 'ayahi wa sallam*) alikuwa akiingia chooni, mimi na kijana mmoja tulikuwa tukimshikilia kata ya maji na mkuki katika kila upande (huku na huku), nae akatekeleza istinjaa kwa maji."** Ulikuwa mkuki ukikitwa ardhini kisha ukiekewa nguo juu yake, mpaka ikawa amefichika na macho ya watu.

Na iwapo akifaulu kujitahirisha kwa kutumia mawe au kitu chochote badala yake, kama vile makaratasi ya chooni na mifano ya hayo, kitendo chake kinajuzu na kinakubalika. Ushahidi wa jambo hilo umetokamana na riwaya Al-Bukhaaree kutoka katika hadeeth ya Abu Hurairah (*radyAllaahu 'anhu*), yakwamba alisema: **"Nilimuandama Mtume (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) alipokuwa anakwenda kukidhi haja yake, nae alikuwa hageuki. Basi nikajisongeza karibu nae mara akasema: 'Hebu niletee mawe ili niyatumie kujipangusia nayo (nijisafishie nayo), na usiniletee mifupa yoyote wala kinyezi.' Nikamletea baadhi ya mawe (niliyoyakusanya) kwenye pambizo ya nguo yangu na nikamuekea kandoni mwake. Kisha nikageuka upande mwengine na alipokwisha kumaliza shughuli yake hiyo, akayatumia (kujisafishia nayo)."** Unapotumia mawe, istinjaa haijuzu ikifanywa kwa idadi ya chini ya mawe matatu kutokana na hadeeth iliyopokewa kutoka kwa Salmaan (*radhiAllaahu 'anhu*) aliyesema: **"Rasoolullaah (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) ametukataza sisi kuelekea Qibla tunapokidhi haja kubwa au ndogo. Na (akatukataza sisi) kufanya Istinjaa kwa mkono wa kulia na kutumia idadi ya chini ya mawe matatu tunapofanya istinjaa."** Imepokewa na Muslim.

Vilevile imetokana na riwaya iliyopokewa na Al-Bukhaaree kutoka kwa Ibn Mas'ood (*radhiAllaahu 'anhu*) yakuwa amesema: **"Mtume (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) alikwenda kukidhi haja kubwa basi akaniamuru mimi nimletee mawe matatu."**

Linalopendekezwa zaidi ni kutumia mchanganyiko wa maji na mawe. Lakini iwapo jambo hilo litakuwa na uzito basi maji yatakuwa ni bora kwa sababu huondoa kabisa alama zozote za uchafu. Mtu asitumie mkono wake wa kulia anapozisafisha najisi zitokazo kwenye sehemu zake za siri, kutokana na hadeeth iliyotangulia kutoka kwa Salmaan (*radhiAllaahu 'anhu*).

Pia haifai kwa mwanamume kuishika tupu yake ya mbele kwa mkono wake wa kulia wakati anapoqidhi haja ndogo (anapokojoa). Hii imetokana na riwaya iliyopokewa na Al-Bukhaaree na Muslim kutoka kwa Abu Qataadah yakwamba Rasoolullaah (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) amesema: **"Na asiiguse mmoja wenu tupu yake (ya mbele) kwa mkono wake wa kulia wakati anapokojoa. Na wala asijipanguse (asinawe) mmoja wenu kwa mkono wa kulia wakati wa kukidhi haja kubwa."**

Vilevile, imeharamishwa kwa Muislamu kunawa (istinjaa) kwa kutumia kinyezi au mifupa au kitu chenye utakaso kutokamana na hadeeth iliyotangulia ya Salmaan, na pia hadeeth ya Jaabir (*radyAllaahu 'anhu*) ipatikanayo katika Saheeh Muslim: **"Rasoolullaah (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) ametukataza kujipangusa kwa kutumia kinyezi kikavu au mifupa (tunapokidhi haya zetu)."**

Sababu ya kuharamishwa huku imetajwa katika Saheeh Muslim kutoka katika hadeeth ya Ibn Mas'ood ni kwamba mifupa ni katika chakula cha Majini. (Pindi mifupa iwafikiapo wao), Allaah (Subhaanahu wata'aalah) Huivisha (au Huijaliza mifupa hiyo) nyama zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Na ama kuhusiana na kinyezi (choo), hivyo ni vyakula vya wanyama wao au vipando vyao.

Jambo hili limefanana na chakula cha mwana-adamu na chakula cha wanyama wao au vipando vyao - hairuhusiwi kwa Muislamu kufanya istinjaa kwa kutumia vitu hivyo.

Hatimae, mtu anapoazimia kutoka nje ya mahali pa kukidhi haja, na aseme yale yaliyo saheeh na kupokelewa kwenye Sunan ya Abu Dawood kutoka katika hadeeth ya 'Aa'ishah: **"Kila wakati Mtume (*sallAllaahu 'alayhi wa sallam*) anapotoka nje ya mahali pa kukidhi haja, husema: '*Ghufraanaka*.'"** Maana yake ni: Nakuomba Msamaha Wako. Sababu ya kufanya hivi nikwamba kwa vile Allaah Amempumzisha kutokamana na kitu chenye madhara (kinyezi), hapo ni mahali pa kisawasawa vilevile Amuombe amuepushie na madhara ya madhambi.

Usoolus-Sunnah:

Amesema Imaam Ahmad Ibn Hanbal: "Asili ya Sunnah kwetu sisi ni aathaar (masimulizi) ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sallallahu 'alayhi wasallam) na sunnah hufasiri na kubainisha Qur'an. Nayo (Sunnah) ni muelekeo katika kuifahamu Qur'an (ni yenye ushahidi na ishara kuhusu makusudio yake na tafsiri swaheeh). Hakuna kujadiliana wala kulinganisha kwa kutumia vipimo vya akili kwenye sunnah. Na haipatikani wala haifahamiki kwa kutumia akili na matamanio. Bali (asili yake) ni kuifuata , kujitegemeza nayo na kujiepusha na hawaa. Na ni kutokamana na kujifungamanisha na sunnah zilotulazimu , (Sunnah) ambazo kwa yeyote atakae puuza jambo lake moja, basi huwa amepinga yote (kwa-ujumla), wala yeye si miongoni mwa walioiamini na pia si miongoni mwa watu wake.

Usoolus-Sunna # 7-13